

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED



## TAARIFA KWA UMMA

# SHINDANO LA WASICHANA KATIKA TEHAMA

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inawaalika wanafunzi wasichana wote wa vyuo vikuu nchini kushiriki katika shindano la Ubunifu linalohusisha uwasilishaji wa wazo lenye ubunifu zaidi linaloleta suluhisho katika jamii, wazo linalowasilishwa linapaswa kuzingatia dhima ya Siku ya Wasichana na TEHAMA 2024 isemayo "Uongozi"

Shindano hili linalenga kumpatia kila mmoja fursa ya kushiriki, kuonesha ujuzi, na kufurahia ubunifu, uvumbuzi na hatimaye kukuza weledi wa uongozi katika TEHAMA.

### Sifa za Mshiriki

- Awe mwanafunzi wa kike Mtanzania anaesoma katika chuo kikuu.
- Awe na ujuzi wa msingi wa kutumia programu za usimbaji (coding) Mfano: Python na R.
- Awe na umri kuanzia miaka 18 hadi 24.
- Uanachama katika Klabu ya Kidijiti ni sifa ya ziada.

Washiriki wanatakiwa kuwasilisha maombi yao kwa njia ya mtandao kupitia kiunganisho kifuatacho <https://edodoso.gov.go.tz/index.php/824558?newtest=Y&lang=en>

**Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 12 Machi, 2024.**

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia namba [0800008272](tel:0800008272) au barua pepe [dawatilahuduma@tcra.go.tz](mailto:dawatilahuduma@tcra.go.tz).

Imetolewa tarehe **28 Februari, 2024**

Mha. Mwesigwa Felician  
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**

Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.

Simu: +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 Nukushi: +255 22 2412009-10

Barua pepe: [barua@tcra.go.tz](mailto:barua@tcra.go.tz), [dg@tcra.go.tz](mailto:dg@tcra.go.tz), Tovuti: [www.tcra.go.tz](http://www.tcra.go.tz)